


A motorcyclist transports conduit pipes in style along a road at Kinondoni in Dar es Salaam yesterday. Photo: Guardian Correspondent




A commuter bus waits for passengers along Goba Road at Mbezi Luis in Dar es Salaam city yesterday even as a signpost in the area bars vehicles from stopping there. Photo: Correspondent Sabato Kasika

The Guardian | THURSDAY 6 August, 2026



Guess what 'daredevil' could be transporting this bulky cargo of empty plastic containers this way along the traditionally busy Jangwani Valley stretch of Dares Salaam city's Morogoro Road, as captured yesterday afternoon! Photo: Correspondent Imani Nathaniel

# Takwa jipya uendeshaji magari ya biashara laleta uhaba madereva

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

Miaka minne tangu Serikali ianze kutekeleza utaratibu wa kuwathibitisha madereva wa magari ya biashara kwa kuwataka kurudi darasani na kufanya tathmini ya ujuzi kabla ya kuendelea na kazi, hali hii sasa imeleta changamoto mpya katika sekta ya usafirishaji.

Hiyo ni baada ya madereva wengi kushindwa kukidhi vigezo vya kufanya kazi hiyo hali iliyoibua uhaba wao sokoni kiasi cha kuanza kuathiri usafirishaji, magari kuegeshwa kwa kukosa madereva.

Hali hiyo imeleta ugumu sasa katika usafirishaji wa mizigo kutoka eneo moja kwenda lingine hasa katika kipindi hiki ambacho utendaji wa bandari ya Dar es Salaam ikishuhudia ongezeko la mizigo.

Januari 7, 2020, Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (Latra) ilianzisha rasmi Kanuni za Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu wa Vyombo vya Moto Kibiashara za mwaka 2020 kupitia gazeti la serikali namba 81 la Januari 7, 2020.

Ili kusimamia utekelezaji huo, Juni 2022 Latra ilianza rasmi kupokea maombi ya madereva kufanya mitihani ya uthibitishaji, ambapo madereva wa magari ya biashara walitakiwa kufanya mtihani huo kabla ya kupata cheti cha uthibitisho.

Utekelezaji wake umekuwa shubiri ambapo Katibu na Msemaji wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (Tatoa), Rahim Dosa anasema tangu agizo hilo lianze madereva wamekuwa adimu hali iliyofanya baadhi ya wamiliki kuegesha magari.

"Mfano mimi gari zaidi ya 30 zipo karakana hazina madereva na wakati huohuo mengine tumeyanunua kwa mkopo, hivyo inakuwa ni hasara kwetu," anasema Dosa.

Hali hiyo imefanya sasa kuwapo kwa ugumu na ucheleweshaji katika usafirishaji wa mizigo ya wafanyabiashara hususani kutoka jiji la Dar es Salaam kwenda maeneo mengine jambo linalodumaza biashara.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Taifa (JWT), Hamis Livembe anasema wanaathiriwa na hali hiyo kwani mzigo wa mtu unapoingia nchini au kutoka mkoa mmoja mfanyabiashara anatakiwa aupate kwa wakati.

"Ukweli ni kwamba idadi ya magari yaliyopo haiendani na idadi ya madereva wanaotakiwa kwa sasa na tunaiomba serikali kulifikiria hilo katika kulitatua ili tuondokane na hali hii," anasema.

Hali hiyo haiathiri wamiliki na wafanyabiashara wakubwa pekee bali hadi mama ntilie walio karibu na maeneo yaliyozungukwa na bandari kavu na kampuni za usafirishaji.

Mariam Juma ambaye ni mama ntilie eneo la Mabibo anasema amelazimika kupunguza kiwango cha chakula anachopika kutokana na kupungua kwa madereva na wasaidizi wao katika eneo la karibu.

"Magari mengi yameegeshwa, madereva hawapo, wasaidizi hawapo, hali hii imefanya tupunguze kipimo cha chakula tunachopika ili kuepusha hasara," anasema.

Uhaba huu unaonekana wakati ambao Bandari ya Dar es Salaam imeendelea kuimarisha nafasi yake kama lango kuu la biashara kwa Afrika Mashariki na Kati baada ya kuhudumia tani milioni 33.7 za mizigo katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Ukuaji huo unaonyesha matokeo ya maboresho ya miundombinu, ongezeko la ufanisi wa huduma na kuvutia mizigo zaidi ya ndani na ya nchi zinazotumia bandari hiyo kama lango la biashara.

**'Kwa sasa mhitimu akimaliza cheti chake mpaka kihakikiwe na kuidhinishwa na jeshi jambo ambalo linaweza kuchukua mwezi hadi miezi miwili kutegemea na taarifa za dereva husika kama zimeshajitosheleza."**

Meneja Uhusiano na Masoko Veta, Sitta Peter

### Msako hadi vyuoni

Wakati upatikanaji wa madereva ukiwa mgumu, Mwenyekiti wa Chama cha Malori ya Kati na Madogo (Tamstoa), Chuki Shabani anasema katika kujinasua alianza kutembelea vyuo vya madereva ili kujua nini tatizo na kubaini chuo cha Veta tawi la Chang'ombe kulikuwa na shida ya kuwapatia vyeti madereva kwa wakati waliokwishamaliza masomo yao.

"Uhaba kweli upo lakini upande wa vyuo walivyoenda kusoma nako tumegundua kuna shida na ndio maana huku mtaani hawaonekani kutokana na kutopewa vyeti pale wanapohitimu hasa walioenda VETA," anasema.

Akijibia suala hilo Meneja wa Uhusiano na Masoko wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Sitta Peter anasema awali dereva alipohitimu alipewa cheti huku Jeshi la Polisi likiwafanyia majaribio mwisho wa mafunzo yaliyowapa uwezo wa kutambuliwa na mamlaka za kutoa leseni.

"Kwa sasa mhitimu akimaliza cheti chake mpaka kihakikiwe na kuidhinishwa na jeshi jambo ambalo linaweza kuchukua mwezi hadi miezi miwili kutegemea na taarifa za dereva husika kama zimeshajitosheleza," anasema.

### Mabasi nao kilio

Uhaba wa madereva umegusa pia Wamiliki wa Mabasi (Taboa) ambapo Katibu wake Priscus Joseph anasema huenda hali ikazidi kuwa mbaya zaidi baada ya bandari ya Dar es Salaam, Tanga na ile ya Mtwara kuboreshwa hali inayoongeza ukuaji wa biashara hususani katika sekta ya uchukuzi.

"Tulikuwa na madereva wazuri zaidi ya miaka 20 hawajawahi kupata hata ajali lakini kutokana na utaratibu huo wa kusoma ulioletwa na serikali wameondoka na kubaki wapya walioenda shule ambao wamekuwa wakiangusha zaidi magari," anasema.

### Walichosema madereva

Wakati wamiliki wakilia uhaba, Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Masafara marefu, malori na mabasi Tanzania (TLDTA) Hassan Dede anasema madereva wapo kinachotakiwa ni wamiliki kuwalipa vizuri.

"Pia sio kwamba madereva hamna watu wameona wafanye shughuli nyingine kwani haiwezekani mfanyakazi wa ndani alipwe kima cha chini Sh300,000 na dereva alipwe hiyo, kuna kampuni huwezi kukuta wanalalamika hawana madereva, kwa sababu wanawalipa vizuri," anasema.

Dede anasema ni wakati madereva waheshimike na kulipwa vizuri kama wa nchi jirani ikiwamo Zambia ambapo anasema mshahara wa dereva ukiacha marupurupu mengine anapokea sio chini ya Sh1.8 milioni jambo ambalo hata Tanzania inawezekana kama litasimamiwa.

Katika kuwapandisha hadhi madereva wanasema kampuni inayohitaji dereva itapaswa kumlipa mshahara sio chini ya Sh700,000.

Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Madereva Tanzania (TADWU), Ramadhan Selemani, anasema suala la madereva kwenda shule haliepukiki na kubainisha kwamba wanaolalamika hawana hela ya kufanya hivyo ni waongo.

"Madereva hawa wanaolalamika hawana Sh300,000 ya kwenda kusoma ndio hawahawa wapo tayari kuhonga si milioni moja kupata leseni kwa njia ya uani au kupata kazi kwenye kampuni, lakini linapokuja suala la kwenda shule anakuambia hana hela, hii sio sawa," anasema Selemani.

